






LISTEN TO "MITIKI YETU" ON RADIO PAMBAZUKO 89.5 FM EVERY FRIDAY 19:30-20:00 & SATURDAY 07:30-08:00

KVTC SINCE 1992

## From Irvine's desk

**CORONA INAUWA, OSHA MIKONO MARA KWA MARA**

Ni mda sasa tangu mpate jarida letu. Ni vizuri kuchelewa kuliko kukosa kabisa. KVTC ina miaka 30 mwaka huu. Miaka 30 baadae, mradi wa kijani sasa umefanikiwa kuwa mmoja kati ya kiwanda endelevu cha msitu ikiwa na wateja wa kuaminika kutoka nchi tano tofauti na imetengeneza ajira za moja kwa moja na zisizo moja kwa moja zaidi ya 600. Kwa sasa tunahaja ya kusherekea.

## Chirag Builders Ltd (www.chiragbuilders.co.ke)

Na Irvine Kanyemba & Niral Fatania

Kampuni ya ujenzi ya Chirag (Chirag Builders Ltd) kutoka Kenya ni kampuni inayo husiana na ujenzi na huduma za ujenzi na iko kwenye biashara kwa miaka 30. Inatoa huduma ya kunatisha ndani kwenye sekta mbalimbali ikiwemo ofisi, matibabu na sekta ya hospitali.

Kampuni ya ujenzi ya Chirag inaelekea kutumia mtiki katika miradi yake mingi. Na hiyo mitiki itatoka KVTC.



.

## KVTC yatoa Jengo la kusetiri wasafiri kwa uwanja wa ndege Ifakara

Na: Kennedy Haule

Uwanja wa ndege wa Ifakara ni kati ya viwanja 58 vinavyomilikiwa na serikali ya Tanzania (GoT) na kusimamiwa na mamlaka ya viwanja Tanzania (TAA). uwanja ulianzishwa mwaka 1956 kabla ya uhuru.

Umbali wa barabara kutoka Dar Es Salaam mpaka Ifakara ni karibu Kilometa 320. Inachukua masaa kumi kuendesha kutoka Dar Es Salaam hadi Ifakara wakati kwa ndege ni s aa moja kwa kuruka.

Njia ya kukimbilia ni mita 1480 urefu na upana ni mita 40 na ni wa kokoto. Uwanja una uwezo wa kuchukua caravans 14 na ATR42s 3 kwa mara moja.

Shirika la Hifadhi ya Taifa Tanzania (TANAPA), Mamlaka ya Wanyama pori Tanzania (TAWA), Kampuni ya ndege Auric Air, Pelican Air, Taasisi ya Wanyama ya Frankfurt (Frankfurt Zoological Society), Jambo Aviation ndio watumiaji wa nzuri wa anga wa kiwanja cha ndege cha Ifakara. Abiria wengi wanauhusiano na kampuni ya mitiki (KVTC), Taasisi ya afya Ifakara, Hospital ya Mtakatifu Francis. Watalii wa TANAPA na TAWA.

Uwanja haukuwa na sehemu ya kuwasetiri abiria na mali zao. KVTC ikaamua, kwa kiasi kikubwa kupitia jitihada za bodi ya wakurugenzi Balozi Ami Mpungwe, kujenga jengo litakalo jumuisha sehemu ya kupumzika , choo na kisima cha maji

Jengo hili lina hifadhi vifaa vya zima moto.



Esther Mwigune Meneja wa TAA Morogoro aliyepokea msaada huu kwa niaba ya Mkurugenzi Mkuu wa taa alishukuru kwa msaada na akawakaribisha wadau wengine nao kujitokeza kuchangia.

## Cleria Atilio Kahemela

**(Meneja Msaidizi Bustani )**



Mwaka 1993 katika halmashauri ya manispa ya Iringa, familia ya Kahemela ilipata thawabu ya kupata mtoto kwa jina la Cleria. Mvuto wake kwenye kusomea misitu ulianza akiwa mtoto kwa kuwa wazazi wake kutokea utotoni walikuwa wanakuza miti.

Cleria ana taaluma ya afisa misitu akiwa amehitimu digrii ya sayansi ya misitu chuo

kikuu cha Sokoine Morogoro. Kama sehemu ya kukamilisha digrii yake ya sayansi ya misitu alifanya andiko la mradi maalumu juu ya mchango wa mashamba ya msitu ya Sao Hill katika Maisha ya jamii inayozunguka mashamba hayo.

Cleria alijiunga na KVTC Oktoba 2020 kwa mafunzo. Na amepata ujuzi juu ya usimamizi wa bustani, upandaji miti, upunguziaji miti, kupunguzia matawi, upembuzi wa udongo, kuandaa muundo wa barabara, kuitafsiri, ujenzi, na utunzaji. Cleria sasa amaeajiriwa kama Meneja Msaidizi Bustani.

Anataka kufanya kazi kwa bidii kwa maendeleo ya KVTC na vilevile kuchangia kuzuia ongezeka la joto duniani. Uvunaji wa kupitiliza misitu kuliko tokana na ongezeko la watu katika ulimwengu mzima kumechangia kuongezeka kwa joto duniani. Kama Afisa Misitu, atawaelimisha watu juu ya uhitaji wa kupanda zaidi miti na uhifadhi wa mali asili.

Cleria anpenda kusoma vitabu vyenye hamasa na hadithi, kusafiri, kusikiliza mziki na kusaidia wenye uhitaji.

## KVTC- Kama Raia hai katika Wilaya ya Ulanga.

**Na: Jeremiah M. Gumadi**

### *Mbio za Mwenge*



Mwaka 2021 Mwenge wa uhuru uliwashwa na kukimbizwa rasmi chini ya baraka za Rais Hussein A. Mwinyi Kusini Unguja Zanzibar Mei 17, 2021 sehemu aliye zaliwa Rais Samia S Hassan. Kauli mbiu ni "***Tehama ni Msingi wa Taifa Endelevu; Itumike kwa Usahihi***".

Wilaya ya Ulanga ni moja kati ya wilaya 150 za kiutawala ambao Mwenge wa Uhuru ulikimbizwa. Agosti 5, 2021, Mwenge wa Uhuru uliwasili Ulanga ukitokea wilaya ya Kilombero.

Mkuu wa Wilaya Ulanga Mheshimiwa Ngollo N Malenya aliongoza ujumbe wa mbio za Mwenge chini ya uongozi wa Kanali Josephine P. Mwambashi kwenda Bustani.Hotuba fupi kuhusiana na shughuli zinazofanyika bustani zilisomwa na Meneja wa Bustani Jeremiah Gumadi

Baada ya hotuba ujumbe ulitembelea bustani kujiridhisha na uzalishajishaji kwa vikonyo (clones), miche na vipande vya kupandia (STUMPS). Mkuu wa msafara alitoa mbegu kwa shule 4 na wanavijiji 5 kama ishara ya uhifadhi wa mazingira kabla ya kupanda mti wa mtiki wa ukumbusho

Tukio hili lilifungwa kwa ujumbe wa pongezi kutoka kwa mkuu wa msafara juu ya kazi ambazo KVTC ina fanya. Uongozi wa KVTC uliwakilisha kinyago cha mbao ya mtiki kilichochongwa picha ya Mwenge kwa mkuu wa msafara na vishikio vya simu 6 vya mbao za mtiki.

## Maonesho ya Biashara ya Ulanga Iherepa

KVTC kama mmoja wa jamii ya wafanya biashara katika wilaya ya Ulanga tulishiriki katika maonyesho ya kukuza fursa za uwekezaji kwa jina ***Ulanga Iherepa*** **(Ulanga inavutia)**. Mkuu wa Wilaya Mh. Ngollo N. Malenya aliandaa tukio la siku mbili Oktoba 22 – 23, 2021. Mgeni rasmi alikuwa Mh. Doto M. Biteko, Waziri wa Madini.



Maonesho yalipambwa na shughuli mbalimbai zikiwemo michezo kama mbio, ngoma za asilia na utalii wa hifadhi ya Taifa ya Nyerere kwa boti na magari.

Fursa ya uwekezaji katika madini yenye thamani (Gemstone) na madini ya lisasi (Graphite) kilimo, misitu ya kibiashara na sekta ya utalii ilionyeshwa.

KVTC ilishiriki na iliweza kuonyesha mnyololo wa kuongeza thamani kutoka bustani, uboreshaji wa miti kupitia uzalishaji wa bidhaa zilizo kamilika kwa mfano zilizo mbao chanwa, milango, paneli, za sakafu na T & g kwa kusakifia. Programu ya kusaidia wakulima wa nje kwa muundo mpya ulielezwa kwa waliotembelea.

## Kiwanda cha Kuongeza Thamani (VAM)

Na: Gustav Sahlertz

KVTC inajivunia yenyewe kwa kutengeneza bidhaa zenye thamani kubwa na ubora kama vile T &G kwa kusakifia. za mapampo zenye kingo 4 pembezoni (E4E) paneli zilizounganishwa pembeni na gundi. (EGP) na milango ya (mbao na paneli). Zilipoingizwa sokoni hizi bidhaa zilipata mvuto na mahitaji yamezidi kuimarika hususana kwa sakafu na mapambo / kunatisha. Na mteja anaridhika na kutokana na uthabiti wa kukausha kwa mbao za KVTC, Wateja wanahakikishiwa na bidhaa imara na inayohimili. Na muonekano wa mng'aro wa dhahabu, mtiki unajitokeza kwa uhakika wakati mbao imekaushwa vizuri.

Mazao ya KVTC's ya kuwa maarufu zaidi katika masoko ya hoteli za kitalii kwa pande mbili Kenya na Tanzania.

KVTC inajivunia kuonyesha vipaji vya hapa kwetu kwa kushirikiana na kampuni kwa kufanya majukumu maalumu. Baadhi ya kazi za usanii ilikuwa inahitajika kwa mbio za mwenge wa uhuru 2021 katika sherehe kama zawadi kwa waheshimiwa na watu maarufu. Mbao maalumu iliyokaushwa na kuunganishwa VAM na baadaye kuchongwa na kupambwa na logo ya KVTC na nembo ya mwenge wa uhuru na mzaliwa wetu wa hapa Ifakara Bwana Sabinus Ulele.



